



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI

Siku ya Mazingira Duniani huadhimishwa kila mwaka Tarehe 5 Mwezi Juni ambapo jamii duniani kote inahamasishwa kutunza mazingira dhidi ya changamoto mbalimbali zinazoikabili dunia kwa sasa. Siku hii ni maalumu kwa sababu jamii inapata fursa ya kuongelea maendeleo endelevu ambayo ni rafiki wa mazingira na viumbe vilivyomo duniani.

Kaulimbiu ya mwaka huu 2020 kama ilivyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni **Tuhifadhi Mazingira: Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**. Mazingira ni jumla ya mambo yote yanayomzunguka kiumbe katika maisha yake. Mazingira hujumuisha vitu vya asili kama misitu, milima, maziwa, mabonde, mito na bahari au ya kutengenezwa na binadamu kama vile majengo na viwanda.

Bila kutunza mazingira, binadamu atadhurika kwa sababu anategemea mazingira na viumbe kwa chakula, hewa, maji, malighafi, mikusanyo, tafiti n.k. Hivyo basi, ni muhimu kutambua athari kwenye mazingira mf. Uchafuzi wa hewa, maji na ardhi, athari ya ongezeko la watu kwenye mazingira, ukataji miti/misitu ovyo, mabadiliko ya tabianchi na namna ya kukabiliana nazo. Utunzaji wa mazingira ni muhimu kwa ajili ya ustawi wa viumbe na uhai wao.

Makumbusho ya Taifa la Tanzania inaunga mkono jitihada za Serikali za kutunza mazingira. Makumbusho inafanya kazi za kukusanya, kutafiti, kuhifadhi, kuonesha na kuelimisha jamiii kuhusu urithi wa asili na utamaduni. Urithi wa asili ni pamoja na uoto wa asili na viumbe waliomo kwenye mazingira.

Kazi hizi zinafanyika kupitia vitengo mbalimbali ikiwemo kitengo cha baiolojia (elimu viumbe) ambacho hutafiti na kuhifadhi viumbe kutoka mifumo ikolojia ya maji na nchi kavu. Taarifa za viumbe hutumika kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa viumbe kwenye mazingira, kutambua athari kwa viumbe na mazingira na namna ya kukabiliana na athari hizi.

Kwa mwaka huu, Makumbusho ya Taifa kupitia Kituo chake cha Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni imeandaa programu ya jinsi ya kutengeneza bustani za vipepeo na wadudu wachavushao na usafi wa mazingira kwa lengo la kutunza mazingira na viumbe ambao wanaathirika kutokana na ukataji hovyoy wa miti na uchomaji wa misitu.

Pia, Makumbusho ya Taifa kupitia kituo chake cha Kijiji cha Makumbusho kimeandaa programu ya utunzaji wa misitu na upandaji miti. Katika programu hiyo jamii itaelimishwa juu ya aina mbalimbali ya miti na matumizi yake. Vile vile, jamii inashirikishwa katika kupanda miti katika eneo la Kijiji cha Makumbusho.

Programu hizi zitasaidia jamii kuelewa namna ya kuhifadhi mazingira yaliyoharibiwa. Kaulimbiu ya Makumbusho ya Taifa ni **Kuelimisha Jamii: Kuhifadhi Mazingira na Viumbe.**

Imetolewa na:

Dkt. Noel B. Lwoga
MKURUGENZI MKUU